Uaminifu mbele ya Mungu na Mwanae Yesu.

TAFADHALI BIBLIA YAKO IWE IMEFUNGULIWA NA UJARIBU KUTAFUTA KUMBUKUMBU REJEA ZOTE.

Katika somo hili nataka kuangalia kwa makini katika mambo tuyafanyayo kila siku. Mengine yatakuwa kuhusu Mungu na kuhusu Yesu. Kama vile kuwahubiri wengine au kuwasaidia wagonjwa na wazee. Mengine yatahusu huduma na maongozi ya familia zetu au wale tulio na madaraka nao. Matendo mengine yote yatahusu watu ambao tunakutana nao kila siku, katika kazi, safarini au lolote linaloweza kujitokeza kila siku.

Uaminifu unahusu kutii amri. Juu ya yote kutii amri za Jamii tunamoishi. Wakati mwingine, katika nyakati za Vita na maafa, sheria za Mwanadamu hudharauliwa, lakini mfuasi wa Yesu hakati tamaa kwa majaribu kama hayo kwani sheria zilizotolewa na Mungu na kuelezwa kwa uangalifu na Yesu na Wanafunzi wake, daima huwa mbele ya maisha yao.

Katika somo la awali tayari tumeangalia katika mafundisho ya Zaburi 34 mstari wa 7. Haya ni maneno ya ajabu na ni kwazo kubwa katika wakati mgumu, lakini maneno yale yanatenda pande zote mbili. Iwapo Malaika wa Mungu wako karibu na watu wenye imani katika maisha yao ya kila siku, basi wako pale pia kusikiliza na kuangalia tunapokuwa wajanja na kutokuwa wa kweli, kusema uongo au kuchukua kisichokuwa chetu.

Sasa fuatana nami katika maneno ya Paulo juu ya mada hii. Hebu natuangalie analotaka kusema. Kwanza halafu kwenye Waraka wake kwa Warumi sura ya 12 mstari wa 17. Paulo anasikitika jinsi wale wasio Wakristo wanavyomuona mtu anayemfuata Yesu. Kumbuka kuhubiri sio tu kusema yale tusemayo kwa wengine, ni pamoja na tuyafanyayo na jinsi tunavyoyafanya. Paulo anaendelea katika sura ya 13 mistari ya 12 hadi 14 kwa kutuambia juu ya matendo ya gizani; mambo ambayo watu huyatenda kwa udanganyifu wakifiri kuwa hawataonekana. Yesu alitumia wazo hili akizungumza na Nikodemu. Utayakuta haya katika Injili ya Yohana sura ya 3 mistari ya 19 hadi 21. Malengo ya mfuasi wa kweli wa Yesu ni kufanya mambo yote ambayo kwayo yataonekana katika nuru kamilifu na yawezekuoonekana kwa kila mtu, na Mungu na watu wengine. Je hii sio njia iliyo wazi kabisa ya kufundisha?.

Katika Waraka wake kwa Wafilipi sura ya 4 mstari wa 8. Paulo anatushauri kufanya mambo mengine kama sheria katika maisha yetu. Mambo kama ukweli, uaminifu, haki, usafi, uadilifu, na mambo yenye kuashiria taarifa nzuri. Mambo haya yatajionyesha kwa wengine kwamba kwa hakika tunamfuata Yesu na wakati huo huo kuwa njia madhubuti ya mafunzo. Tunapokuwa tunazungumza kwa majirani zetu juu ya Yesu na Injili yake ya Ufalme, watakuwa tayari kuamini tunayoyasema.

Inashangaza kusoma katika nyaraka za Paulo na Petro kuhusu inavyotupasa kuwa kwa wale wanao tutawala. Serikali zinatofautiana katika dunia hii, baadhi ni nzuri baadhi zimejaa rushwa, nyingine zina taratibu nzuri za utawala wa haki, nyingine ni za mabavu na ukatili na bado mitume walishauri kuonyesha uaminifu kwa wote wenye madaraka ya duniani. Hebu angalia katika Waraka wa kwanza wa Paulo kwa Timotheo sura ya 2 mistari ya 1 hadi 3. Maneno haya yaliandikwa wakati utawala wa Kirumi ukikazana kuwatesa Wakristo. Aghalabu yalikuwa mafundisho magumu kuyakubali na kuyaweka katika vitendo lakini pia yako pale kwa ajili yetu kuyafuata. Yesu aliwafundisha wanafunzi wake kulipa kodi kwa Mtawala wa Warumi na katika maneno yake litupatia jambo moja la ziada la kukumbukwa. Hebu natuangalie maneno ya Yesu kama ilivyoandikwa na Mathayo katika sura ya 22 mistari ya 17 hadi 22. Maelekezo ni kutoa kwa jamii tunamoishi, malipo ya kodi na ushuru, lakini kwa Mungu tuonyeshe upendo wetu kwake na kutoa maisha yetu katika kumtumikia.

Tulipoangalia ushauri wa Paulo alioutoa kwa Wakristo wa Wafilipi , je ulitambua maneno yoyote yenye sifa njema. Mambo ambayo kwa kawaida yalikubalika na wote kuwa ni mwafaka kwa wafuasi wa Yesu kuyafanya. Mambo ambayo haikuwa mtu mmoja aliyeamua bali uamuzi wa Wajumbe wa Kanisa wanaoaminika. Kuna mfano mwingine kama huo ambapo maoni ya Wanafunzi wenyeji wote yalitumika. Uko katika Matendo ya Mitume sura 6 mstari wa 3. Wengine, Kwa wakati ule ilikuwa muhimu kuwachagua watu wazuri zaidi walipokutana. Hawa wangekuwa mashemasi,viongozi na waongozaji wa wengine. Pengine ulikuwa ni uchaguzi mzuri uliofanywa kwa sababu tunazo habari za wawili tu kati ya watu hawa ambao walionekana kuwa watumishi wazuri wa kanisa watawala wenye uwezo wa kuongoza na wahubiri hodari. Somo la kutoka agano jipya limerudiwa mara kwa mara ″ Fuata mafundisho ya Yesu na maelekezo na maelezo makini ya wanafunzi” Ingawaje kuna ushauri huu wa kibiblia, kama kawaida tunawategemea marafiki na wale tuliozoeana nao kwa ushauri wa kibinadamu.

Je umewahi kufikilia ni nini kinachosababisha hata ushauriwe na mtu mwingine ili ukubali ushauri wao? Pengine ni wazee wenye uzoefu mkubwa katika maisha, wenye busara au waaminifu.Natuangalie mifano miwili ya watu waliotoa ushauri. Mfano wa kwanza

tunaukuta katika kitabu cha hesabu sura ya 13 katika mpaka wa nchi ya ahadi Musa alikuwa amewatanguliza mbele ya taifa zima la israeli wapelelezi kumi na mbili ukisoma mistari ya 26 hadi 33 utaona taarifa ya wapelelezi inayofuatana. Kumi walirejea wakijawa na hofu na mashaka, na wawili tu ndiyo walikuwa na imani na uhakika kwamba mbele ya Mungu hakuna lisilowezekana. Sasa soma katika kifungu cha 14 na kwa uangalifu angalia maneno ya Kalebu na Joshua katika mistari ya 6 hadi 9. Ni nani unadhani watu hawa walimwamini? Ni bahati mbaya kwa wale kumi ambao hawakumwamini. Hasira ya Mungu kuambatana na uchaguzi wao inatuonyesha ni nani kati ya hao kumi na wawili walikuwa waaminifu, wakutegemewa na wenye imani. Walikuwa ni Kalebu na Joshua mshahara wao ulikuwa ni kuvuka hadi katika nchi ya Ahadi na familia yao ambapo wale wote waliokosa imani walifariki Jangwani.

Mfano mwingine wa marafiki waliotoa ushauri unapatikana katika Kitabu cha Ayubu 42 mistari ya 7 hadi 10. Ilikuwa sawa kwa Ayubu kudharau ushauri wa Mwanadamu na badala yake kuzingatia imani katika Mungu. La muhimu kubaini ni kwamba watu wale watatu walijaribu kumsaidia Ayubu na walitumia muda mwingi wakijaribu kumliwaza katika huzuni aliyokuwa nayo, sura ya 2 mstari wa 13.

Tatizo lao ni kuwa katika ushauri wao hawakutumia njia na maadili ya Mungu. Badala yake walitumia ubinadamu na hekima za mwanadamu. Hii ni tofauti ambayo hatuna budi kuangalia tunapopewa ushauri kutoka kwa marafiki. Mambo mengine yanayohusu uaminifu yanaonekana kuwa hayana maana, lakini kwa Mungu hata yale madogo tunayoyafanya ni muhimu kwake. Sasa anglia Unabii wa Mika sura ya 6 mstari wa 8. Baadhi ya mifano inapatikana katika mistari ya 10 na 11.

Hebu fikiria mizani ya Wafanyabishara iliyorekebishwa kwa makusudi ili kupima kiasi kidogo cha bidhaa kisicholingana na kiasi kinacholipwa na mteja. Mfanyabishara atajifikiria kuwa ni mjanja na mwelevu lakini Mungu anamchukia Mfanyabishara huyu aliyejificha. Aidha yawezekana usiwe Mfanyabiashara, lakini je maneno haya yatakuhusu vipi? Katika maisha yetu tunawafanyia mambo wengine, aghalabu tuna ajira; katika mambo yote haya tunaweza kutumia nguvu zetu kwa bidii au kidogo tu. Tunaweza kulipwa au kutokulipwa mshahara wetu. Hali kadhalika tunapomtendea Mungu, tunaweza kumtolea zaidi au kidogo tu katika wakati na nguvu zetu. Udanganyifu unatokea tunapojifanya kwa Wakristo wenzetu kuwa tunajitolea vyote tulivyonavyo. Tunapokuwa tumepewa madaraka juu ya wengine au madaraka ya fedha, tunapaswa kukumbuka sana somo hili. Hata kama tutapata majaribu ya kutumia vibaya madaraka yetu, Mungu atajua tunachofikiria na tunatarajia kufanya nini kwa siri. Inawezekana kuficha matendo yetu kwa watu wengine lakini haiwezekani kuyaficha kwa Mungu. Somo hili linafafanuliwa barabara katika Matendo ya Mitume sura ya 5 mistari ya 1 hadi 11. Hapa mtu na mkewe walijaribu kumdanganya Mungu na Mitume. Mshahara wao wa udanganyifu ulikuwa mchungu na mkubwa. Unaweza kuona kwamba hii ni sawa kabisa na Utukufu wa kuwa na mizani au vipimo vya udanganyifu mahali pa soko na tunasoma katika Mika kwamba Mungu analichukia hili.

Matukio ya Anania na Safira bila shaka yalikuwa mabaya kiasi cha kupelekea hatua za haraka kuhitajika kwani ni tukio la kipekee katika Agano jipya ambapo nguvu za Roho Mtakatifu zilitumika katika kutoa uhai. Katika hali nyingine zote ilitumika kuponya na hata kuwafufua wale waliokuwa wamefariki.

Wakati Yesu aliporuhusu achukuliwe na askari, kupigwa na halafu kusulibiwa, alijitolea kila kitu kwetu. Aliyafanya haya ili watu waume kwa wanawake wawezeshwe kuwa na njia iliyofunguliwa na hatimaye kuokolewa kutoka katika uharibifu wa kifo. Hakukuwa na udanganyifu katika Yesu, daima alikuwa mwaminifu kamili na muwazi kwa wote waliomwendea. Katika mafundisho yake kuhusu misha ya Mkristo , alitupatia vipimo maalumu vya malengo yetu katika kumfuata. Angalia Injili ya Luka sura ya 6 na soma mistari ya 35 hadi 38. Maneno ya mwisho katika mstari wa 38 yanatukumbusha haja ya kujitolea kwa uaminifu iwapo tunataka kuupokea urithi wa Ufalme.

CBM Publishing, 32 Blenheim Rd, Far Cotton, Northampton NN4 8NW United Kingdom
PO Box 2950, Mbeya, Tanzania (East Africa)